



Jumuiya ya Madola ya Massachusetts

Idara ya Elimu na Utunzaji wa Mapema

Sera	
Agizo la Ukaguzi wa Rekodi ya Historia katika Kielekezi cha BRC kwa Aina zote za Mpango	Shughuli za Nje– Mipango Yote Iliyoidhinishwa na Kufadhiliwa
Tarehe ya Kuanza: Jumanne, 22 Agosti 2023	

Agizo la Ukaguzi wa Rekodi ya Historia katika Kielekezi cha BRC

Wakati mteuliwa anafaa kufanyiwa ukaguzi wa rekodi ya historia (BRC) kupitia Idara ya Elimu na Utunzaji wa Mapema (EEC), uwasilishaji huanzishwa katika Tovuti ya Mpango wa BRC (mfumo wa Kielekezi). Barua ya arifa ya alama za vidole hutumwa kwa mteuliwa kupitia barua pepe (iliyo na kitambulisho cha kipekee cha uandikishaji) na inamwagiza mteuliwa achukuliwe alama za vidole.

Baada ya mteuliwa kuchukuliwa alama za vidole, ukaguzi wa BRC uliosalia utaendeshwa kwa wakati mmoja:

- Taarifa za Rekodi za Wahalifu wa Jinai (CORI),
- Taarifa za Usajili wa Wahalifu wa Makosa ya Ngono (SORI), na
- Idara ya Watoto na Familia (DCF).

Inapohitajika, ukaguzi wa ziada ufuatao utatekelezwa:

- Rekodi ya Kitaifa ya Wahalifu wa Ngono (NSOR) kwa wateuliwa fulani (wale walio chini ya mamlaka ya CCDBG), na
- Rekodi ya Wahalifu wa Jinai ya kila jimbo, Rekodi ya Ustawi wa Mtoto na Rekodi ya Wahalifu wa Ngono hukagua mteuliwa yeyote ambaye anaishi au ameishi nje ya jimbo katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita.
 - Wafanyakazi wa mpango wa makazi ambao wanaishi au wameishi nje ya nchi katika miaka 5 iliyopita watakamilisha tu ukaguzi wa Ustawi wa Mtoto.

Ni lazima wateuliwa wote waweke miadi ya kuchuliwa alama za vidole kwa haraka iwezekanavyo ili kuharakisha mchakato huu. Mteuliwa yeyote ambaye hajachukuliwa alama za vidole ndani ya miezi minne (4) ataghairiwa kiotomatiki kutoka kwa mfumo wa EEC BRC na atahitaji kuingizwa tena na mpango na kujaza fomu mpya ya idhini.

Hali ya kusimamiwa na ya muda ya GSA na Mpango Unaofadhiliwa

Kwa Wateuliwa wa Kikundi na Umri wa Shule (GSA) na wa Mpango uliofadhiliwa, baada ya mteuliwa kuchukuliwa alama za vidole na kukamilisha ukaguzi unaohitajika wa wahalifu wa ngono, EEC hukamilisha mchakato wake wa uchunguzi wa awali na inaweza kuidhinisha mpango wa kuajiri wateuliwa fulani chini ya hali inayosimamiwa na ya muda.

Mteuliwa anapoajiriwa kwa muda, mpango unaweza kumtumia mteuliwa huyu katika mpango wake wakati usimamizi ni wa moja kwa moja na wa mara kwa mara. Mfanyakazi yeyote wa mpango ambaye ana ufaafu wa sasa wa EEC anaweza kutekeleza kazi hii ya usimamizi. EEC mwanzoni huarifu mpango tu wakati mteuliwa anastahiki hali ya muda. Punde tu programu inapobadilisha hali ya kuajiri ya mteuliwa kuwa “aliyeajiriwa kwa muda,” mteuliwa pia huarifiwa (kupitia barua pepe). Mteuliwa anaweza kufanya kazi chini ya hali ya kusimamiwa na ya muda hadi wakati ukaguzi uliosalia wa mteuliwa huyo ukamilike, muda wa siku 120, na Mpango kupokea uamuzi wa mwisho wa ufaafu wa mgombea huyo kutoka kwa EEC.

Wateuliwa wafuatao **hawastahiki** kusimamiwa, hadhi ya muda chini ya hali yoyote: wenye leseni, wateuliwa wa malezi ya watoto wa familia, wateuliwa wa makazi na upangaji, walezi wa familia, walezi wasio wa familia, wafanyakazi wa shirika, wafanyakazi wa usafirishaji, mipango na watu wanaohusishwa, wa muda. wafanyakazi wa shirika wa muda, na watoa huduma wenye kandarasi. Lazima wateuliwa hawa wachukuliwe kuwa “wanafaa” kikamilifu na EEC kabla ya kufanya kazi katika mpango wowote iliopewa leseni au kufadhiliwa na EEC kwa nafasi yoyote.